# MWONGOZO WA RIDHAA INAYOTOLEWA KWA UHURU, KABLA NA BAADA YA KUPATA TAARIFA ZA KUTOSHA

OXFAM

Kimechapishwa mara ya
kwanza Juni 2010
Kimechapishwa tena
Aprili 2014
Oxfam Australia
132 Leicester Street
Carlton Victoria
3053 Australia
Simu: +61 3 9289 9444
Faksi: +61 3 93471983
www.oxfam.org.au

**Waandishi:** Christina Hill, Serena Lillywhite na Michael Simon
**Mchangiaji:** Chelsea Huggett na Claire Hussin
**Mhariri:** Jane Kunstler
**Msanifu:** Kate Bensen
**Mfafanuzi:** Katie Webber
**Uchapaji:** Eduardo Carbonell

## SHUKURANI:

Oxfam ingependa kutambua na kuzishukuru asasi nyingi na watu binafsi ambao walitoa ushauri na mwongozo katika maandalizi ya chapisho hili. Hasa tunapenda kutambua ushauri na mchango kutoka katika Programu ya Watu wanaoshughukia Msitu, Mito ya Kimataifa, Taasisi ya Rasilimali za Duniani, Oxfam Amerika, Shirika la Kikatoliki kwa ajili ya Maendeleo ya Nchi za Ng'ambo na Mkataba wa Wenyeji wa Asia . Tunapenda pia kutambua Mfuko wa Planet Wheeler kwa msaada wao wa fedha.

Uandaaji wa mwongozo huu wa FPIC ulisaidiwa na program ya msaada ya Australia, iliyofadhiliwa na Idara ya Maaendeleo ya Mambo ya Nje na Biashara ya Australia.

Australian Government
Department of Foreign Affairs and Trade

Australian AID

© Oxfam Australia 2014

Oxfam Australia inahusiana na Baraza la Australia la Maendeleo ya Kimataifa (ACFID), ambayo tunafungwa na kanuni zake za maadili; Oxfam International, ambayo tunafungwa na katiba yake na kanuni za maadili; Watu Wanaopata Msaada, ambao tunafungwa na kanuni zao; na Baraza la Wakimbizi la Australia.

Ripoti hii inapatikana kwenye mtandao www.oxfam.org.au/explore/mining/free-prior-and-informed-consent

# YALIYOMO

UTANGULIZI ..... 4

UFAFANUZI WA MANENO MUHIMU ..... 8

KUPANGA TUKIO: KWA NINI MWONGOZO HUU NA KWA NINI SASA? ..... 10

KUIELEWA FPIC: RIDHAA INAYOTOLEWA KWA UHURU,
KABLA NA BAADA YA KUPATA TAARIFA ZA KUTOSHA ..... 11

FPIC ILITOKA WAPI? INAFANYA KAZI KWA NANI? ..... 12

HATUA ZA UTENDAJI: FPIC INATUMIKAJE KULINDA HAKI ZAKO? ..... 13

WAPI TUTAKAKOWEZA KUPATA MSAADA NA TAARIFA ZAIDI?
NANI MWINGINE ANAYESHUGHULIKIA MASUALA YA MALIASILI? ..... 30

KIAMBATISHO CHA 1: ..... 32

KIAMBATISHO CHA 2: ..... 33

KIAMBATISHO CHA 3: ..... 34

# UTANGULIZI

Oxfam inatambua changamoto na masuala ya usalama ambayo jamii nyingi na watu binafsi wanakabiliwa nazo katika kuhakikisha haki na kero zao zinatambuliwa na kuzingatiwa. Katika kutumia mwongozo huu, jamii zinashauriwa kuzingatia kwa makini hatari zozote za usalama wanazoweza kukabiliwa nazo.

## LENGO LA MWONGOZO WA RIDHAA INAYOTOLEWA KWA UHURU, KABLA NA BAADA YA KUPATA TAARIFA ZA KUTOSHA

Mwongozo huu ni utangulizi wa Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha (FPIC). Unatoa taarifa ya msingi kuhusu haki ya FPIC na jinsi haki hii inavyoweza kusaidia watu kuwa na uamuzi kuhusu miradi ya maendeleo, kama vile mabwawa, machimbo na ukataji wa magogo na miradi mingine mikubwa ya miundombinu, ambayo inawaathiri kwa namna fulani.

Sisi sote tuna haki ya kuamua kinachotokea katika ardhi zetu. Kanuni hii inalindwa na sheria ya haki za binadamu ya kimataifa inayosema 'watu wote wana haki ya kuamua wenyewe' na kuhusishwa na haki ya uamuzi binafsi, 'watu wote wana haki ya kufanya kwa uhuru maendeleo yao ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Mwongozo umeandaliwa kwa ajili ya kusaidia asasi zinazosaidia jamii zilizoathiriwa na miradi mikubwa ya maendeleo. Ni zana halisi ya kuwezesha mazungumzo kati ya jamii na waanzishaji wa miradi — ikiwa ni pamoja na makampuni, serikali na wagharimiaji.

Mwongozo huu una muundo wa hatua saba ambao unakusudia kuwasaidia Wenyeji walioathirika na mradi kuungana na kutoa madai ya haki zao za FPIC. Unaorodhesha pia kanuni kama zinavyotumika kwa jamii zote zinazoathirika na miradi. Unayo pia sehemu ambayo ni kama rasiliamali kwa ajili ya kuzisaidia jamii kuelewa haki zao na vidokezo vinavyofaa na taarifa. Mwongozo pia una 'bendera nyekundu' ambazo zinafafanua kinachoweza kwenda vibaya na ugumu ambao jamii zinaweza kukabiliana nao.

## UTANGULIZI WA FPIC

Wenyeji wanapambana kutambuliwa na serikali za taifa lao, jumuiya ya kimataifa na kampuni juu ya haki yao ya kukubali au kukataa kutoa ridhaa kwa uanzishaji wa mradi wa maendeleo. Haki hii inahusiana moja kwa moja na haki ya wenyeji kudhibiti siku zao zijazo na siku zijazo za watu wao. Imekuwa ikitamkwa kama haki ya kutoa au kukataa 'kutoa ridhaa yao inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha katika vitendo ambavyo vinaathiri ardhi, maeneo na maliasili zao'.

Hii imefupishwa na kuwa Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za kutosha,au FPIC.


Haki hii mara nyingi inavunjwa kunapokuwa na miradi mikubwa ya maendeleo — kama machimbo ya madini, mabwawa, barabara kubwa, mashamba au ukataji wa magogo. Mara nyingi wenyeji na wanajamii wao wanaachwa nje ya mchakato wa mipango na kufanya uamuzi katika miradi hii. Matokeo yanaweza kuwa makubwa. Wenyeji na jamii zinazoathirika na mradi zinapata hasara ya kudumu ya utafutaji wao wa riziki na utamaduni. Ardhi zinaweza kuharibiwa au kuchukuliwa bila ridhaa yao. Uhamaji mara nyingi unalazimishwa kwa jamii na kutolewa kwa fidia ndogo.

Hili haliwezi kutokea. Wenyeji wanalindwa dhidi ya hali hii chini ya sheria ya Kimataifa na Azimio la Umoja wa Mataifa linalohusu Haki ya Wenyeji (UNDRIP). Ulinzi pia unapatikana kwa ajili ya jamii nyingine zilizoathirika na mradi. Wenyeji wana haki ya kushirikishwa katika uamuzi wowote ambao unaathiri ardhi zao, maliasili au maeneo yao. Wana haki ya kukubali au kukataa kutoa Ridhaa yao inayotolewa kwa Uhuru, kabla na baada ya kupata Taarifa za kutosha. Wanayo haki ya kutoa au kukataa Ridhaa yao kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha. Wanayo haki ya kufikia uamuzi wa pamoja kupitia michakato inayotambulika na kuamuliwa na wao wenyewe.

Kwa jamii zisizo za wenyeji zilizoathirika na mradi, ushiriki wao kamili na wenye ufanisi katika makubaliano na mipango ya mradi lazima uungwe mkono.

### Hatua ya 1

Kutafuta nani anaanzisha mradi



### Hatua ya 2

Kuomba taarifa kutoka kwa mwanzishaji wa mradi




### Hatua ya 3

Kufanya majadiliano na jamii yako




### Hatua ya 4

Jamii kufanya majadiliano na waazishaji wa mradi



**Hatua ya 5**

Kutafuta ushauri huru




**Hatua ya 7**

Mawasiliano yanayoendelea na waanzishaji wa mradi



**Hatua ya 6**

Kufanya uamuzi kama jamii



## CHANGAMOTO

Kudai haki ya Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata taarifa za Kutosha inaweza kuwa kazi yenye changamoto. FPIC ni mchakato unaoendelea na majadiliano yanaweza kuchukua miaka kadhaa. Jamii zilizoathirika kutokana na mradi zinaweza kudai ushiriki wao katika mapatano, au katika suala la jamii za wenyeji, ambapo haki yao katika FPIC inaheshimiwa. Haki hizi mara nyingi hazitambuliwi moja kwa moja. Baadhi ya Serikali, kampuni na wagharimiaji wamepiga hatua katika kuheshimu haki hizi — na wana sera na wajibu ambao unapaswa kutumika wanapoanzisha mradi. Lakini kwa waanzishaji mradi wengi FPIC bado ni kitu wasichokiheshimu, hawakitekelezi wala kukielewa kikamilifu.

Pia, kunaweza kuwa na sheria za taifa katika nchi ambazo zinabadilisha namna FPIC inavyoweza kudaiwa. Ni muhimu kwa jamii zilizoathirika kutokana na mradi kupata ushauri kuhusu sheria za ndani ya nchi yao.

## NANI MWENYE HAKI YA RIDHAA INAYOTOLEWA KWA UHURU, KABLA NA BAADA YA KUPATA TAARIFA ZA KUTOSHA?

FPIC ni haki maalumu kwa Wenyeji kama inavyotambuliwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa linalohusu Haki za Wenyeji (UNDRIP). Tazama Kiambatisho cha 1 katika ukurasa wa 32 kwa ajili ya orodha ya nchi zinazounga mkono UNDRIP.

Oxfam Australia ina mtazamo kwamba jamii zote zilizoathirika kutokana na mradi zina haki ya ushauri na majadiliano katika mchakato wa kufanya uamuzi unaowaathiri. Watu wasiokuwa wenyeji, walioathirika kutokana na mradi wana haki ya ushauri na majadiliano katika mchakato wa kufanya uamuzi katika njia ambazo zina mfululizo mzuri pamoja na kanuni zilizomo ndani ya haki ya FPIC.

Kwa madhumuni ya mwongozo huu, jamii zote zilizoathirika kutokana na mradi zinajumuishwa, bila kujali iwapo wao ni jamii za Wenyeji au Wasiokuwa wenyeji. Hii inazingatia kuhusu uelewa kwamba haki za jamii zote haziwezi kuzingatiwa sawa na haki za Wenyeji kwa kuzingatia ridhaa. Hata hivyo, jamii zote zilizoathirika kutokana na mradi lazima ziweze kushiriki katika ufanyaji uamuzi na majadiliano yenye ufanisi na wakati jamii za wasiokuwa wenyeji

zinaposema 'hapana' katika mradi hili linapaswa kuzingatiwa. Swali lililopo katika kiambatisho cha 2 (ukurasa wa 33) litakusaidia kuelewa iwapo haki yako ya FPIC imelindwa katika sheria ya taifa nchini mwako.

# UFAFANUZI WA MANENO MUHIMU

### Faida

Kitu kizuri ambacho kinatokana na mradi kwa ajili ya jamii. Kinapaswa kujadiliwa kati ya jamii na waanzishaji wa mradi au serikali.

### Benefit sharing

Njia ya kuhakikisha faida za mradi zinagawanywa sawa mingoni mwa jamii zilizoathirika.

### Ridhaa

Kutoa au kukataa makubaliano kwa ajili ya mradi kuendelea kwa mwanzishaji wa mradi.

### Ushauri

Wakati mwanzishaji wa mradi na jamii wanaposhirikishana taarifa na kuzungumza kuhusu mradi uliopangwa. Ushauri ni tofauti na ridhaa.

### Haki ya pamoja

Haki ya kikundi cha watu, kama vile jamii. Sio haki ya mtu mmoja binafsi.

### Azimio

Katika mfumo wa Umoja wa Mataifa (UN), ni tamko la nchi za dunia. Halifungwi kisheria. Linapanga kanuni ambazo serikali zinakubali kukusudia kuzifanyia kazi. Linaweza kufungwa kisheria kama litaingizwa katika sheria za nchi.

### Mchakato wa kufanya uamuzi

The way in which your community chooses to decide whether to give or deny your consent for stages of the project.

### Kukosa makazi

Watu kupoteza makazi na ardhi zao.

### Kukosa njia za kiuchumi

Kukosa kipato au utafutaji wa riziki kunakotokana na kupoteza ardhi.

### Wasomi kuteka mradi

Umiliki wa kujadiliana faida zinazopatikana pamoja na mwanzishaji wa mradi kufanywa na 'wasomi' wachache au watu wenye nguvu kwa ajili ya faida zao binafsi badala ya faida ya jamii nzima.

### Tathmini ya athari kwa mazingira na jamii

Utafiti unaofanyika kabla ya kuanza kwa mradi kuangalia madhara yanayoweza kutokea kutokana na mradi unaopendekezwa. Lengo lake ni kuzuia madhara kwa watu na mazingira yao.

### Madhara

Matokeo ya mradi mkubwa wa maendeleo ambayo yanaathiri jamii vibaya. Mfano: uchafuzi wa mto, kukatwa kwa msitu, kuhamishwa kwa kijiji. Ni gharama ya mradi iliyoathiri jamii, na sio mwanzishaji wa mradi.

### Makubaliano ya faida zinazoweza kusababisha madhara.

Makubaliano ya kisheria kati ya jamii na mwanzishaji wa mradi ambayo yanaonyesha masharti ambayo mwanzishaji wa mradi lazima ayatekeleze.

### Sheria ya kimataifa

Sheria ambayo inaongoza uhusiano kati ya nchi mbalimbali. Katika eneo la haki za binadamu inaweza kupanuka hadi namna ambayo nchi zinawatendea watu binafsi na jamii.

### Maliasili

Kwa mwanzishaji wa mradi ni chanzo cha suala la kimazingira ambalo linaweza kuchukuliwa kwa ajili ya kufaidika kiuchumi, kama vile mbao, mafuta na maji. Kwa ajili ya jamii, ni chanzo cha utafutaji riziki, kama vile maji kwa ajili ya kunywa, ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

### Majadiliano

Majadiliano kuhusu masharti ya makubaliano yaliyofanyika katika mchakato wa haki, kwa kawaida ni kati ya mwanzishaji wa mradi na jamii zilizoathirika. Kunapaswa kuwa na uwiano wa madaraka. Mradi haupaswi kuendelea hadi majadiliano yakamilike.

### Asasi Isiyo ya Serikali (AISE)

Asasi ambayo ni huru dhidi ya serikali. Sio kampuni. Hii inaweza kuhusisha asasi za dini (kama vile makanisa) na asasi nyingine za kiraia na kijamii.

### Mwanzishaji wa Mradi


Benki, kampuni au serikali inayotaka kuanzisha mradi. Mara nyingi kuna pande nyingi zinazoshirikishwa katika kuanzisha mradi

### Makazi mapya

Kuondolewa na kupelekwa katika eneo jipya la kuishi na kutafuta riziki ili kuacha eneo kwa ajili ya kuanzishwa kwa mradi mkubwa wa maendeleo. Wakati mwingine uhamishaji unasimamiwa na serikali ya nchi kwa niaba ya waanzishaji wa mradi.

### Vihatarishi

Uwezekano wa kuumia, kupoteza au hatari. Uhatarishi unaweza kutokea kwa watu binafsi au jamii nzima. Waanzishaji wa mradi pia hukabiliwa na uhatarishi, kwa mfano kuharibika kwa heshima kama walishirikishwa katika ugomvi au migogoro na watu walioathirika kutokana na mradi.



# KUPANGA TUKIO: KWA NINI MWONGOZO HUU NA KWA NINI SASA?

Miradi ya miundombinu mikubwa duniani na viwanda vya uchimbaji vimekuwa vikianzishwa kwa haraka sana. Miradi hii imesukumwa na mahitaji yasiyoongezeka ya maliasili. Hizi ni pamoja na ukataji wa magogo na miti ya mbao, uchimbaji wa madini na mafuta, na uchimbaji wa mabwawa na kuchepusha mito kwa ajili ya umeme

unaotengenezwa kwa maji. Inaweza kusababisha mabadiliko makubwa katika maisha ya watu, hali yao ya utafutaji wa riziki na mazingira ndani ya eneo na kuzunguka eneo la mradi.

Kama itaanzishwa kwa uendelevu, miradi hii inaweza kuwa na faida kwa wenyeji. Miradi hiyo inapaswa kuepuka athari hasi ya kimazingira na kijamii, na kutokuleta madhara.

Lakini mara nyingi sana miradi inasababisha matatizo na athari hasi, yanayodumu kwa muda mrefu, ikiwa ni pamoja na haki za binadamu. Moja kati ya sababu kubwa ni kwamba inaanzishwa bila kuwa na uzingatiaji wa haki na masilahi ya watu walioathirika na mradi na mazingira.

Kuna njia nyingi tofauti ambazo miradi mikubwa ya maendeleo inaweza kuathiri jamii yako. Baadhi ya madhara ya mradi yanayoweza kutokea ni:

### Athari chanya au faida

- Ajira nyingi kwa wanajamii
- Mafunzo ya ujuzi
- Mifumo mizuri ya usambazaji wa maji na maji taka
- Uzalishaji wa chakula ulioboreshwa
- Faida za kifedha
- Shule mpya, kliniki za afya na nyumba

### Athari hasi au madhara

- Wasiwasi wa kuondoka katika ardhi yako
- Kuzuiliwa kuifikia ardhi iliyotumika kwa uzalishaji wa chakula au vitendo vya kiutamaduni
- Kuchafuliwa kwa maji na hewa yenu
- Kupotea kwa samaki, wanyama au mimea katika eneo lenu
- Kuongezeka kwa vurugu na msongo wa kijamii
- Mara nyingi kazi ni za muda mfupi
- Wafanyakazi wanaokuja katika eneo la mradi wanasababisha hatari za kiafya kwa jamii

Ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha ni haki muhimu ya pamoja ambayo inaweza kusaidia kufanya miradi kuwa endelevu zaidi. Inaweza kudaiwa na wenyeji mahali ambapo mradi unaathiri maisha yao, utafutaji wa riziki, au ardhi na maeneo yao. Kwa jamii nyingine zilizoathirika na mradi, ushiriki wao kamili na wenye ufanisi katika majadiliano dhidi ya mipango na utekelezaji wa miradi hii lazima uhakikishwe.

Hata pale ambapo sheria za taifa zinatoa ulinzi hafifu wa haki ya FPIC, na haki ya watu walioathirika kutokana na mradi kupata ushauri na kushiriki katika mchakato wa kufanya uamuzi, haki hizi zinaweza na zinapaswa kutambuliwa na waanzishaji wa miradi.

Mwongozo huu unakusudia kuzisaidia jamii zote zilizoathirika kutokana na mradi kuelewa vizuri FPIC na jinsi inavyofanya kazi. Inakusudia kuwapa baadhi ya rasilimali na msaada katika kulinda haki zao pale mradi unapopendekezwa katika eneo lao. Ni nyenzo kwa ajili ya jamii kuwabana waanzishaji wa mradi na serikali kuwajibika.

# KUIELEWA FPIC: RIDHAA INAYOTOLEWA KWA UHURU, KABLA NA BAADA YA KUPATA TAARIFA ZA KUTOSHA

Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za Kutosha (FPIC) inahusu jamii ya wenyeji kuwa na haki maalumu ambazo wengine wanapaswa kuziheshimu. Ni haki ya pamoja. Hii inamaanisha jamii yako kwa ujumla, ina haki ya kukubali au kukataa kutoa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za Kutosha.

Kila sehemu ya neno ina maana yenye umuhimu kwako na kwa jamii yako. Ufuatao ni ufafanuzi rahisi wa maana ya kila neno:

- **Huru** bila ya kulazimishwa, kutumia vitisho, kutumia nguvu au kushinikizwa na serikali au kampuni.
- **Kabla** ya serikali kutenga ardhi kwa ajili ya matumizi fulani na kabla ya kuthibitishwa kwa miradi maalumu. Unapaswa kupewa muda wa kutosha kuzingatia taarifa zote na kufanya uamuzi.
- **Taarifa za kutosha**, unapaswa kupewa taarifa zote muhimu ili kufanya uamuzi wako kuhusu iwapo ukubali au ukatae mradi (tazama ukurasa wa 18 na 19 kwa ajili ya orodha ya maswali ya kuwauliza waanzishaji wa mradi). Pia:
  - Taarifa hizi lazima ziwe katika lugha ambayo unaweza kuielewa kwa urahisi.
  - Unapaswa kupata taarifa huru, sio mradi ni taarifa kutoka kwa waanzishaji wa mradi au serikali yako.
  - Lazima pia upate taarifa kutoka kwa wataalamu wa sheria na masuala ya kitaalamu, kama wakiombwa, kukusaidia kufanya uamuzi wako.
- **Ridhaa** inataka kwamba watu waliohusika katika mradi waruhusu jamii za wenyeji kusema 'Ndiyo' au 'Hapana' katika mradi na katika kila hatua ya mradi, kwa mujibu wa mchakato wa ufanyaji uamuzi wa uchaguzi wako. Haki ya kutoa au kuzuia ridhaa ndio tofauti iliyo muhimu sana baina ya haki za Wenyeji na watu wengine walioathirika kutokana na mradi.

Kwa watu wasiokuwa wenyeji haki yako ya ushauri na majadiliano katika mchakato wa kufanya uamuzi unaokuathiri unapaswa pia kuongozwa na kanuni za FPIC. Ushauri na majadiliano yanapaswa kufanyika pale tu unapokuwa hujalazimishwa au kushinikizwa kushiriki , kabla ya uamuzi uliofanyika na ridhaa inapaswa kufanyika tu unapokuwa na taarifa za kutosha kuhusu masuala yaliyojadiliwa na kukubaliana.

FPIC inalinda haki za jamii za kujadiliana katika uamuzi unaowaathiri. Hii inamaanisha kwamba inaweza kuwa mchakato wa kawaida wa kufanya uamuzi. Baadhi ya jamii zinachagua wawakilishi wa jamii kujadiliana na mwanzishaji wa mradi kwa niaba ya jamii

**Kumbuka: kukusaidia kuelewa FPIC, inashauriwa kwamba utumie muda kusoma kila ibara ya Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Wenyeji.**

> Jamii zinahitaji kulindwa dhidi ya waanzishaji wa mradi ambao wanaweza kujaribu kuanzisha utaratibu wao wenyewe wakati mchakato wa kawaida wa ufanyaji uamuzi ambao tayari upo.

# FPIC ILITOKA WAPI? INAFANYA KAZI KWA NANI?

Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za Kutosha ni haki inayotambuliwa katika sheria ya kimataifa. Imejumuishwa katika sheria za nchi kwa baadhi ya nchi — kama vile Ufilipino na katika sehemu za Australia (ingawa sheria zinaweza kubadilika kati ya nchi na majimbo).

FPIC pia inatambuliwa kama tendo zuri katika miradi ya maendeleo. Inaweza kuzifaidisha kampuni zinazowekeza katika miradi mikubwa ya maendeleo. Kwa mfano, inaweza kupunguza uwezekano wa kutokea kwa mgogoro kati ya jamii na kampuni kama jamii zinashiriki kikamilifu katika kufanya uamuzi wa mradi kutoka mwanzoni. Aidha,serikali inaweza kufaidi katika kulinda haki hii ya watu wake.

Chati mtiririko ifuatayo inatoa mwonekano rahisi wa mahali FPIC ilikotoka na inafanya kazi kwa nani:

**JAMII**

**Wenyeji wana haki ya FPIC. UNDRIP Ibara ya 32(2):**
'Nchi zinapaswa kushauriana na kushirikiana kwa uaminifu na wenyeji wanaohusika kupitia taasisi zinazowawakilisha ili kupata RIDHAA INAYOTOLEWA KWA UHURU, KABLA na BAADA YA KUPATA TAARIFA ZA KUTOSHA kabla ya kuidhinisha mradi wowote unaoathiri ardhi au maeneo yao'.

**Azimio la UN kuhusu Haki ya Maendeleo:**
'Kila mmoja ana haki ya maendeleo'. Uendelevu wa maendeleo unahusishwa na uwezo wa watu kudhibiti malengo ya maendeleo yao. Ushiriki wa jamii katika mradi unaowaathiri unapaswa kufuata utaratibu pamoja na kanuni za msingi za FPIC.

**Waanzishaji wa mradi lazima walinde na kuheshimu haki hizi na kanuni zinazohusiana nazo katika kazi zao zote.**


**Sheria za taifa**
Wakati mwingine haki hizi, ikiwa ni pamoja na haki ya FPIC, zinalindwa katika sheria ya taifa.

**MAENDELEO ENDELEVU**

**Zingatia: Mswada wa Kimataifa wa Haki — unajumuisha Azimio la Dunia la Haki za Binadamu, Makubaliano ya Kimataifa ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni, Makubaliano ya Kimataifa ya Haki za Raia na Kisiasa, na Makubaliano ya msingi ya Shirika la Kazi Duniani — zote zinafaa kwa matumizi ya kanuni za FPIC kwa watu wote**

walioathirika na mradi.

# HATUA ZA UTENDAJI: FPIC INATUMIKAJE KULINDA HAKI ZAKO?



## HATUA YA 1

### Tafuta nani anaanzisha mradi uliopangwa

Kwanza, nani anapanga mradi ambao unaweza kuiathiri jamii yako. Kisha utajua ni watu gani wanaopaswa kukuomba ridhaa yako.

Wapangaji wa mradi na waanzishaji wanaweza kujumuisha:

- serikali yako;
- kampuni binafsi (kama vile ya uchimbaji madini au ujenzi);
- serikali ya nchi nyingine;
- mamlaka ya ndani ya nchi (kama vile Shirika la Kulinda Mazingira au Idara ya Mazingira na/au Maliasili; na
- benki au taasisi ya kimataifa ya fedha (kama vile Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Asia au Benki ya Maendeleo ya Afrika).

Wakati mwingine inaweza kuwa vigumu kupata taarifa kuhusu mwanzishaji wa mradi. Miradi mikubwa kwa kawaida inashirikisha mchanganyiko wa masilahi binafsi na ya serikali. Kama una matatizo kupata taarifa kuhusu mradi, unaweza kupata msaada kutoka katika asasi nyingine, ikiwa ni pamoja na AZISE za ndani ya nchi na za kimataifa. Vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na magazeti ya kimataifa na majarida ya tasnia hiyo (kwa mfano majarida ya uchimbaji madini) yanaweza pia kuwa na taarifa kuhusu miradi iliyopangwa.

Wakati mwingine waanzishaji wa mradi hawatoki nchini kwako. Hii inaweza kusababisha ugumu zaidi kuwasiliana nao na unaweza kuhitaji msaada kutoka kwa wengine.

# WHO IS RESPONSIBLE?




**Mara nyingi waanzishaji wa mradi na wale wenye wajibu wa kutafuta ridhaa ni muunganiko wa asasi zote zilizotajwa hapo juu.**

**KIDOKEZO CHA 1:**
: Tafuta kama kuna asasi yoyote ambayo inasaidia kusimamia ardhi au rasilimali katika nchi zote za karibu. Kwa mfano, kunaweza kuwa na asasi inayosimamia mto ambayo inafanya kazi katika kila nchi ambayo mto huo unapita. Kama ipo, hakiki kama serikali yako ni sehemu ya asasi hiyo. Kama una wasiwasi kuhusu mradi wa bwawa unaweza kuwa na uwezo wa kutafuta zaidi kuhusu mradi pamoja na msaada wao.




## HATUA YA 2

### Kuomba taarifa kutoka kwa waanzishaji wa mradi

Ni muhimu kufahamu jinsi mradi uliopendekezwa utakavyoathiri jamii yako. Kisha unaweza kutoa uamuzi baada ya kupata taarifa za kutosha kuhusu:

- kutoa au kukataa kutoa ridhaa;
- mabadiliko ambayo ungependa katika mtindo wa mradi; na
- masharti ya awali unayohitaji kuona yametimizwa kabla ya kukubaliana na mradi.

Baadhi ya njia ambazo kwazo mradi unaweza kuathiri jamii zimewekwa katika sehemu ya 'Upangaji wa onyesho: kwa nini mwongozo huu na kwa nini sasa?' katika ukurasa wa 10.

Kama unadhani jamii inaweza kuathirika na mradi, unayo haki ya kuuliza au kupewa taarifa kutoka kwa waanzishaji wa mradi katika lugha yako. Ni muhimu kwa jamii yako kuwa na taarifa za kutosha kuhusu mradi, ni madhara gani yanayoweza kutokea na mwanzishaji wa mradi atafanya nini kuzuia au kuyapunguza.

Kuomba nakala za tathmini ya madhara kimazingira na kijamii katika lugha yako ni muhimu sana. Hii inasaidia kuhakikisha wanajamii wote wana taarifa za kutosha na kuelewa uwezekano wa kutokea kwa madhara. Inasaidia pia kuzuia mchakato wa majadiliano 'kutekwa' na wanajamii wachache ambao wanaweza kuvutiwa zaidi na mradi kwa sababu ya faida binafsi badala ya faida ya jamii.

## Ni muhimu kupata taarifa nzuri kuhusu mipaka ya kijiografia ya mradi na kuhakikisha kwamba mwanzishaji wa mradi anabainisha kwa usahihi jamii zote zinazoweza kuathirika. Kama Mwazishaji wa mradi hajaifikiria jamii yako 'kuwa yenye uwezekano wa kuathirika', mwanzishaji wa mradi anaweza kukwepa kushauriana na kujadiliana na jamii yako.

Njia mojawapo ya kupata taarifa hii ni kumuuliza maswali mwanzishaji wa mradi. Unaweza pia kurekodi taarifa hizi na kuzirejesha kwa jamii yako kwa ajili ya kuijadili. Ukurasa unaofuata unatoa baadhi ya maswali yanayofaa kuuliza.

Unaweza pia kuiuliza moja kwa moja idara ya serikali inayohusika katika nchi yako. Hii inaweza kujumuisha Idara ya Mazingira, Madini, Misitu na Kilimo au Hazina. Hii inaweza kutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine.

Jamii yako inaweza kuathirika hata kama mradi haupo katika eneo lako moja kwa noja. Kwa mfano, uchafuzi wa maji kutokana na maendeleo yanaweza kusambaa na kuathiri jamii inayoishi nje ya eneo la mradi. Au bwawa linaweza kuzuia samaki wanaohama ambayo inaweza kuathiri chanzo chako cha chakula na utafutaji wa riziki.

**Kumbuka: hata mradi ambao upo katika nchi nyingine unaweza kuathiri jamii yako. Kwa mfano, machimbo ya madini katika nchi nyingine yanaweza kutupa taka zake katika mto ambao unatiririka kupitia katika nchi yako na kwamba jamii yako inayategemea maji hayo.**

**KIDOKEZO CHA 2:**
**Unaweza kuomba taarifa kuhusu mradi, katika lugha na muundo ambao unaeleweka kwa jamii yako.**

## BAADHI YA MASWALI YA MSAADA YA KUMUULIZA MWANZISHAJI WA MRADI

### Kuuelewa mradi

- Mradi ni upi? Utafanya nini?
- Mradi ni mkubwa kiasi gani? Utaanza lini? Utafanya kazi kwa muda gani?
- Nani ni waanzishaji wa mradi (kwa mfano kampuni binafsi, serikali)?
- Je, historia au utendaji wa zamani wa kampuni hii ni upi? Je, wana sifa nzuri au mbaya?
- Nani anayetoa mikopo ya uwekezaji (kwa mfano benki ya biashara, Benki ya Dunia, mfuko wa uwekezaji)?
- Je, ni kazi zipi kuu za kila mwanzishaji wa mradi?
- Je, waanzishaji wa mradi ni raia wa wapi?
- Nini kitajengwa kwa ajili ya mradi (kwa mfano barabara, mabwawa, nguzo kubwa za umeme)?
- Nani atashirikishwa katika mradi, zaidi ya kampuni au Serikali (kwa mfano wasambazaji, makandarasi)?
- Je, ni msaada gani ambao Serikali inatoa (kwa mfano hakuna kodi ua kodi iliyopunguzwa kwa ajili ya waanzishaji wa mradi, gharama zilizopunguzwa kwa ajili ya upatikanaji na matumizi ya ardhi)?
- Je, ni maoni gani ya vyombo vya ndani ya nchi vinavyoongoza kuhusiana na mradi?

### Athari ya mradi

- Ni ardhi ipi itakayoathirika?
- Je, kuna ramani yoyote inayoonyesha ardhi iliyoathirika? Je, athari yoyote ya ardhi na rasilimali nyingine zitakuwa za kudumu?
- Je, mwanzishaji wa mradi amefanya tathmini ya athari za haki za binadamu,mazingira, jinsia na jamii?
- Je, zipi ni hatari zinazoweza kutokana na mradi (kwa mfano uchafuzi au kuingia katika eneo la ibada takatifu)?
- Je, kuna ripoti yoyote huru yenye taarifa za kina kuhusu hatari hizi na je zinapatikana kwa ajili ya jamii?
- Je, ni faida gani zitakuwepo kwa ajili ya jamii ya wenyeji? Je, faida hizo zitakuwa za kudumu au za muda?
- Je, kampuni itachangia nini katika jamii (kwa mfano shule, barabara, hospitali na programu nyingine za maendeleo ya kijamii?)
- Je, mradi utachangia kulinda mashamba katika ardhi ya jamii? Kama waanzishaji wa mradi watachukua ardhi yetu itafidiwa ikiwa ni pamoja na kutupatia ardhi mpya?

### Ushauri na majadiliano ya jamii

- Je, ni fursa zipi ambazo jamii inapaswa kupata ili kuchangia katika aina ya mradi? Je, hii itasimamiwa vipi?
- Je, jamii zitashiriki vipi katika mchakato wa tathmini ya athari ya kimazingira na kijamii?
- Nani amefanya tathmini ya athari za mazingira na jamii na je, zitatafsiriwa katika lugha za wenyeji?
- Nani mwenye kampuni iliyotoa ushauri? Je, kampuni inadhani wanayo ridhaa ya jamii?
- Je, ni michakato ipi itafuatwa kama kutakuwa na mabadiliko yoyote katika aina ya mradi?
- Je, kampuni itajadiliana na jamii katika kila hatua ya mradi?
- Je, mwanzishaji wa mradi atajibu vipi kero za jamii?
- Je, mwanzishaji wa mradi yuko tayari kueleza wazi faida na malipo yanayohusiana na mradi?
- Je, faida zinazotokana na mradi zitakwenda wapi?

**Zingatia: Haya ni baadhi ya maswali yaliyopendekezwa. Kutakuwa na maswali mengine mengi ya ku**






## HATUA YA 3

### Fanya majadiliano ndani ya jamii yako

Mara unapokutana na waanzishaji wa mradi, mnapaswa kuanza kujadili kuhusu mradi kwa kina ndani ya jamii yako. Jamii nzima inapaswa kuwa na taarifa za kutosha kuhusu mradi uliopendekezwa. Nyenzo kama vile ramani, brosha, mabango na video zinaweza kutumika kuwafahamisha wanajamii. Hii itasaidia kuhakikisha kila mmoja anaelewa faida zinazoweza kupatikana na athari ambazo mradi unaweza kuwa nazo. Jamii yenu inapaswa kuamua kipi ni muhimu. Kisha wawakilishi wenu wa jamii wanaweza kujadiliana na waanzishaji wa mradi kama hilo ndilo jamii ililoamua kuwa ni hatua inayofuata.

Mnapojadili kile mnachokitaka, tumieni vitendo vinavyokubalika katika jamii yenu kufikia makubaliano. Ni muhimu sana kuzingatia maoni ya wanajamii wote wanaoweza kuathirika. Jaribuni kuhakikisha kwamba wanajamii wote, ikiwa ni pamoja na wanawake na vijana, wanashirikishwa katika michakato yenu ya kutoa uamuzi.Hii ni kwa sababu miradi mikubwa inamuathiri kila mmoja kwa njia tofauti.

Mara nyingi kuna jamii nyingi zinazoathirika na mradi mmoja. Waanzishaji wa mradi lazima wawaambie kuhusu makubaliano yoyote wanayofanya pamoja na jamii nyingine. Inaweza kusaidia kwa jamii yako kuangalia kama jamii nyingine zimeathirika na baadhi ya miradi. Mtaweza kushirikiana kujadiliana na waanzishaji wa mradi au serikali.

Mara nyingi baadhi ya maeneo ya jamii yanaweza kuunga mkono mradi wakati maeneo mengine ya jamii yanapinga mradi. Baadhi ya waanzishaji wa mradi wanaweza kujaribu kuzigawa jamii katika pande mbili ya kundi “linalounga mkono” na “linalopinga”. Hili linaweza kudhoofisha uwezo wa jamii wa kufanya uamuzi

wa pamoja kuhusu mradi na linaweza kusababisha wasiwasi unaoendelea katika jamii.

Inawezekana kwamba jamii mbalimbali zitaathirika kutokana na mradi lakini jamii moja itaathirika zaidi ya nyingine. Kama hali ndiyo hii, ni muhimu kujaribu kuanzisha mbinu ya kawaida pamoja na jamii nyingine ili jamii iliyoathirika vibaya zaidi iwe na sauti yenye nguvu.

**KIDOKEZO CHA 3:**
Hamtakiwi kufanya uamuzi wowote katika hatua hii. Uamuzi wenu wa kwanza unaweza kuwa ni kutaka kupata taarifa zaidi kutoka kwa waanzishaji wa mradi.



## HATUA YA 4

### Majadiliano ya jamii pamoja na waanzishaji wa mradi

Kama jamii, mna haki ya kushauriwa na kujadiliana na waanzishaji wa mradi. Kuzungumza na waanzishaji wa mradi HAKUMAANISHI mnakubali mradi. Mnadai haki yenu ya kupata taarifa kuhusu mradi.

Waanzishaji wa mradi wanapaswa kushauriana na jamii yenu na kupata Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha katika hatua za awali za upangaji wa mradi na kabla ya kila hatua mpya ya mradi. Hii inamaanisha kwamba kama mnakubali katika kipengele cha mradi cha hatua ya kwanza, mwanzishaji wa mradi lazima apate FPIC yenu tena katika hatua inayofuata. Kama kuna uwezekano wa kuhamishwa kwa jamii, kanuni na masharti lazima zijadiliwe pamoja na jamii kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho.

**KIDOKEZO CHA 4:**
**Mwanzishaji wa mradi hapaswi kuwalazimisha kuingia katika mapatano kabla hamjawa tayari kufanya hivyo. W aanzishaji wa mradi lazima wawape muda wa kutosha kuz ingatia taarifa, kuamua namna mnavyotaka kupatana na waanzishaji wa mradi, na mwishokufanya maamuzi kama jamii.**

## Ni muhimu kwamba wanajamii wenu wote washiriki katika majadiliano ya faida na sio viongozi wachache au 'wasomi' ambao wanaweza kuwa na matakwa ya kupata faida zao binafsi kwa gharama ya jamii nzima. Wanajamii wote wanapaswa kulindwa dhidi ya 'kutekwa na wasomi' wa jamii na mchakato wa majadiliano na mwanzishaji wa mradi.

Ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa kawaida unaleta faida kubwa za fedha kwa wawekezaji. Kwa bahati mbaya, jamii za wenyeji sio wakati wote zinapewa fursa za kugawana fedha au faida nyingine. Kuweka vizuri mifumo ya 'ugawanaji wa faida' kunaweza kuhakikisha jamii zilizoathirika kutokana na mradi zinafaidika kutokana na mradi. Kwa mfano inawezesha jamii yenu kuchagua faida inazotaka kupokea. Hii ina uwezekano wa kuboresha utafutaji wa riziki wa jamii yenu. Inaonyesha namna mradi unavyoweza kuongeza thamani katika jamii.

- Baadhi ya mifano ya faida ambayo unaweza kujadiliana kwa ajili ya jamii yenu ni pamoja na:
- Ajira zaidi kwa wanajamii;
- Mafunzo ya ujuzi na programu ya upataji wa kazi;
- Shule na kliniki mpya za afya;
- Upatikanaji maalumu na haki za kutumia rasilimali katika maeneo ya mradi kwa ajili ya jamii zilizoathirika kutokana na mradi;
- Makubaliano na waanzishaji wa mradi kuacha baadhi ya ardhi pasipo kuigusa — kwa mfano, maeneo ya mila za kitamaduni; na
- Kugawana mapato kutokana na mradi.
- Kugawana mapato kutokana na mradi.

**KIDOKEZO CHA 5:**
**Kama ujenzi tayari umeshaanza katika mradi bila kushirikishwa au ridhaa ya jamii, waanzishaji wa mradi wanatakiwa kuambiwa kuwa hawajafuata utaratibu unaokubalika. Bado mnaweza kuwa na la kusema. Bado mnaweza kuzuia ujenzi huo kwa kusisitiza kuwa mwanzishaji wa mradi anaweza kuendelea iwapo tu jami i yenu itatoa Ridhaa Huru, Inayotolewa Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha, kupatana faida kwa ajili ya jamii yenu au kubadilisha namna mradi unavyoendeshwa.**




## HATUA YA 5

### Kutafuta ushauri huru

Kujadiliana na waanzishaji wa mradi kunaweza kuwa na ugumu. Waanzishaji wa mradi wakati mwingine wanajaribu kuepuka kuzishirikisha jamii. Masuala yanayohusishwa ni magumu. Mnayo haki ya kupata ushauri huru wa kisheria na kitaalamu ili kuwasaidia kuzielewa athari za mradi uliopendekezwa. Kwa mfano, kampuni inawafahamisha kwamba watakuwa wakitumia zebaki (mercury). Kama hamjawahi kusikia zebaki au hamjui zaidi kuhusu zebaki, mnaweza kutafuta ushauri kutoka kwa mtaalamu wa sayansi.

Kumbuka kwamba uamuzi wenu lazima utolewe baada ya kupata taarifa za kutosha. Moja kati ya kanuni zinazoongoza za FPIC ni kwamba ridhaa ya Wenyeji inapaswa kutolewa baada ya kupata taarifa za kutosha. Kwa wanajamii wengine wote walioathirika na mradi, ushiriki wao katika ushauri na majadiliano katika michakato ya kufanya uamuzi inapaswa kuzingatia kuwepo kwa taarifa kamili kuhusu masuala yaliyojadiliwa na kupatana.

Ni muhimu kutotegemea taarifa ambazo zinatolewa kwenu na waanzishaji wa mradi pekee. Waanzishaji wa mradi wanaweza kujaribu kufanya mradi uonekane kuvutia kwa jamii zilizoathirika ili kupata ridhaa yao. Taarifa kutoka katika vyanzo vingine vitawahakikishia uelewa wa kutosha wa madhara ya mradi katika muda mfupi na mrefu, na haki gani zilizopo kwa jamii yako.

**Kumbuka: Ni muhimu kutafuta iwapo sheria za taifa lako zinalinda haki zako za FPIC, au michakato kama hiyo ya FPIC. Ushauri huru unaweza kuwasaidia katika suala hili.**

**Kwa taarifa zaidi kuhusu wapi unakoweza kupata ushauri huru, angalia ukurasa wa 30.**

Hata mahali ambapo sheria za taifa zinalinda haki za jamii katika FPIC, mambo bado yanaweza kwenda vibaya. Rushwa, kupata motisha isiyoridhisha au kutopata kabisa, au kukosekana kwa uhuru katika mashirika ya serikali yanayohusika na kuhakikisha kwamba FPIC inafanyika kama inavyotakiwa kisheria, inaweza kusababisha matatizo kwa jamii zinazojaribu kudai haki zao za FPIC.




## HATUA YA 6

### Kufanya uamuzi kama jamii

Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha ni haki ya pamoja. Kwa hiyo, jamii yako lazima ifanye uamuzi pamoja kwa mujibu wa michakato yenu ya mila ya ufanyaji uamuzi.

Kama mtaamua kusema 'ndiyo' katika mradi, mnapaswa kuhakikisha kwamba makubaliano mliyoyafanya pamoja na waanzishaji wa mradi yanarekodiwa kwa maandishi. Mnaweza kuandika hili katika lugha ya/za jamii yenu. Makubaliano haya yanapaswa kufungwa kisheria.

Huu unaweza kuwa mchakato mgumu sana na kuelewa mikataba ya mradi, idhini za serikali na nyaraka za kisheria ni ngumu sana. Inashauriwa kuomba msaada kutoka katika AISE au mtu mwingine mwenye utaalamu unaohusika kuwasaidia kama hamuelewi mikataba na nyaraka nyingine.

Kama jamii yenu itaridhia kutoa ridhaa katika mradi, jamii yenu inaweza kuchagua kuingia katika mkataba ambao utakuwa na athari (au unaofanana na huo) pamoja na mwanzishaji wa mradi. Haya ni makubaliano ya kisheria ambayo yanarekodi makubaliano yaliyofikiwa kati ya jamii yako na mwanzishaji wa mradi. Yanarekodi ni masharti gani ambayo mwanzishaji wa mradi lazima ayatimize na wakati gani masharti haya yatatekelezwa au kuwasilishw.

Baadhi ya waanzishaji wa mradi wanaweza kujaribu kupata 'ridhaa' ya jamii kwa ajili ya mradi kwa kuwalewesha wamiliki wa ardhi na wawakilishi wao na kuwalazimisha kusaini nyaraka.

Baadhi ya waanzishaji wa mradi wanajaribu kupata 'ridhaa' ya jamii kwa ajili ya mradi kwa kuanzisha michakato yao ya kufanya uamuzi. Michakato hii haihusishi miundo ya kimila ya kufanya uamuzi au wawakilishi halali wa jamii na inaandaliwa kwa namna ya kupata 'ndiyo' hata kama mchakato huo ni wa kughushi.

Kumbuka: Kama jamii yako inaamini kwamba mradi hautakuwa mzuri kwa jamii, mnaweza kusema 'hapana' — au kwa maneno mengine msitoe ridhaa yenu — kwa mradi huo. Mradi unapaswa kuendelea iwapo tu ridhaa ya wenyeji imetolewa na wote serikali na mwanzishaji wa mradi. Kwa jamii zisizo za wenyeji zilizoathirika kutokana na mradi wanaposema 'hapana' katika mradi hili linapaswa kuangaliwa.

Kumbuka: Mwanzishaji wa mradi asishinikize, kuwatishia au kuwalazimisha kwa njia yoyote katika kufanya uamuzi au kutoa ridhaa yenu katika mradi. Baadhi ya mifano ya namna waanzishaji wa miradi wanavyofanya mchakato kuwa mgumu ni:

Kutozihusisha jamii katika hatua za awali za tathmini ya athari;

Kuzilazimisha jamii kusaini makubaliano wakati ni wazi kuwa hawaelewi kikamilifu athari za miradi; na

Kujadiliana au kufanya mazungumzo na watu wachache tu ambao hawawezi kuwakilisha maoni ya jamii.




## HATUA YA 7

### Mawasiliano yanayoendelea na waanzishaji wa mradi

Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha ni mchakato endelevu. Miradi mikubwa ya maendeleo inachukua miaka mingi kupanga hadi kuanza, kisha itaathiri jamii yako kwa miaka mingi au hata vizazi . Waanzishaji wa mradi wanapaswa kuhakikisha jamii yako inapata taarifa za kutosha mara kwa mara kuhusu maendeleo ya mradi. Lazima uwe umepata nafasi ya kuuliza maswali na kuibua wasiwasi. Haki ya jamii yako ya FPIC lazima iheshimiwe wakati wote wa mchakato mzima.

Kiambatisho cha 3 katika ukurasa wa 34 kinaainisha awamu za mradi mkubwa. Hii imejumuishwa katika kubainisha umuhimu wa kuelewa shughuli tofauti ambazo zinaweza kutokea katika kila hatua ya mradi, na waanzishaji wa mradi wanapaswa kufanya nini kuzihusisha jamii katika kila hatua.

**Kumbuka: FPIC haipaswi kuwa mchakato wa 'mara moja' ni mchakato unaoendelea. Hii inamaanisha mazungumzo ya mara kwa mara na makubaliano kati ya waanzishaji wa mradi na jamii zilizoathirika ni utendaji mzuri.**

**Kama mtasema 'ndiyo' au 'hapana' kwa mradi, wawakilishi wa jamii wanaweza kuendelea kufanya majadiliano kwa niaba ya jamii yako. Lazima wahakikishe kwamba jamii nzima inapata taarifa za kutosha kwa pamoja.**

**KIDOKEZO CHA 6:**
**Kutafuta asasi huru ya kusaidia kufanya ufuatiliaji kunaweza kusaidia kushawishi waanzishaji wa mradi ambao wana wasiwasi kuhusu madhara ya mradi na wajibu ni halali.**

**KIDOKEZO CHA 7:**

**: Ni muhimu kuelewa na kupatana mkakati uliopo na waanzishaji wa mradi kabla mradi haujaisha. Hii inaweza kujumuisha upataji unaoendelea wa maji safi ya kunywa, utunzaji wa vituo na mafunzo yakuongeza fursa za ajira.**

Wawakilishi wa jamii pia wanahitaji kufuatilia maendeleo ya mradi kama mradi unaendelea. Ni muhimu kwa jamii kufuatilia iwapo kampuni/serikali inatimiza ahadi zake. Njia mojawapo ya kufanya haya ni kukubaliana juu ya matokeo maalumu au masharti ya mradi. Haya yanapaswa kuandikwa na kwa muda uliokubalika.

Mwanzishaji wa mradi anaweza kubadilika kwa kipindi cha uwepo wa mradi. Waanzishaji wapya wa mradi wanapaswa kudumisha ahadi zilizofanywa na waanzishaji wa mradi waliopita — hata hivyo, unaweza kutaka kutafuta ushauri huru ili kuelewa kama mwanzishaji mpya wa mradi anafungwa na makubaliano yaliyopita. Hii ni sababu moja kwa nini ni muhimu kuwa na kumbukumbu zilizoandikwa za uamuzi wa jamii yako kuhusu mradi na faida mlizokubaliana. Mnaweza kupenda kujaribu kupata faida zilizoboreshwa kwa ajili ya jamii yako na mwanzishaji mpya wa mradi.

Jamii yako inaweza pia kutaka kuanzisha mkutano wa kudumu wa jamii na mwanzishaji wa mradi kwa ajili ya mawasiliano ya mara kwa mara. Mkutano huu unaweza pia kutumika kushughulikia wasiwasi au malalamiko ambayo jamii yako inaweza kuwa nayo katika uendeshaji wa mradi kama mradi unaendelea.

> Hatua zilizofafanuliwa hapo juu zimeandaliwa ili kukusaidia wewe na jamii yako kudai haki yenu katika Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha, haki yako ya kuombwa ushauri na haki yako ya kujadiliana katika michakato ya kufanya uamuzi itakayokuathiri.

# WAPI TUTAKAKOWEZA KUPATA MSAADA NA TAARIFA ZAIDI? NANI MWINGINE ANAYESHUGHULIKIA MASUALA YA MALIASILI?

Utafanya nini kama serikali au mwanzishaji wa mradi atakupuuza? Hata kama utajaribu kufuata hatua hizi, waanzishaji wa mradi wanaweza kukupuuza tu na kuendelea na mradi. Unaweza kuamua kuanzisha mkakati wa utetezi unaofaa katika mazingira na jamii yako. Hii inaweza kuhusisha: jamii kupinga, maandamano ya amani ya kupinga yanayofanywa na jamii, na kuibua uelewa kupitia vyombo vya habari na AZISE za nchini na za kimataifa. Baadhi ya AZISE zimeanzisha miongozo inayofaa ya utetezi.

## MAANDIKO MUHIMU

- **United Nations Declaration on Rights Indigenous Peoples (UNDRIP)**
  www.un.org/esa/socdev/unpfii/en/declaration.html
- **Free Prior and Informed Consent: The Role of Mining Companies, Oxfam Australia, 2007**
  www.oxfam.org.au/campaigns/mining/docs/FPIC_statement.pdf
- **Breaking Ground: Engaging Communities in Extractive and Infrastructure Projects; World Resource Institute, 2009**
  www.wri.org/publication/breaking-ground-engaging-communities
- **FREE and EQUAL towards respect for the Human Rights of Indigenous Peoples of Australia: A guide for community advocates, Oxfam Australia and Diplomacy Training Program, 2009**
  www.dtp.unsw.edu.au/documents/FreeandEqual_FALR_002.pdf
- **Dams, Rivers and Rights: An Action Guide for Communities Affected by Dams, International Rivers Network, 2006 (available from website in 10 languages)**
  www.internationalrivers.org/en/node/579/
- **Amnesty International Campaigning Manual, 1997**
  www.amnesty.org/en/library/info/ACT10/002/1997
- **Care Advocacy Tools and Guidelines: Promoting Policy Change, 2001**
  www.care.org/getinvolved/advocacy/tools/english_00.pdf
- **Advocacy for social justice A Global Action and Reflection Guide, 2001**
  www.oxfamamerica.org/publications/advocacy-for-social-justice

## MASHIRIKA

### Umoja wa Mataifa

- **The United Nations Special Rapporteur on the situation of human rights and fundamental freedoms of Indigenous People**
  http://www2.ohchr.org/english/issues/indigenous/rapporteur/
- **The United Nations Permanent Forum on Indigenous Issues**
  http://www.un.org/esa/socdev/unpfii/

### Mashirika yasiyo ya serikali ya Kimataifa

- **Asia Indigenous Peoples Pact**
  www.aippnet.org
- **Catholic Agency For Overseas Development (CAFOD)**
  www.cafod.org.uk
- **Forest People's Program**
  www.forestpeoples.org
- **International Rivers**
  www.internationalrivers.org
- **Oxfam America**
  www.oxfamamerica.org
- **Oxfam Australia**
  www.oxfam.org.au

### Mashirika yaliyopo katika eneo lenu

- Shirika la Masuala ya Kijamii lililo katika nchi yako na AZISE nyingine za nchini
- Mkutano wa AISE au shirika mwavuli katika nchi yako
- Huduma za kisheria za jamii yako
- Mamlaka za ndani (kama vile Shirika la Kulinda Mazingira au Idara ya Mazingira na/au Maliasili)

# KIAMBATISHO CHA 1:

## NCHI AMBAZO ZINAUNGA MKONO AZIMIO LA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU HAKI ZA WENYEJI (UNDRIP)

UNDRIP ni azimio. Katika sheria ya kimataifa hii inamaanisha haifungwi kisheria katika nchi mbalimbali. Bado ni muhimu sana kwani inaweka viwango vinavyotambuliwa na kukubalika na jumuiya ya kimataifa na serikali mbalimbali.

Kama nchi yako imeunga mkono azimio hilo, inapaswa kuwajibika kufanya kazi kwa kuzingatia ulindaji wa haki hizo.

Chati mtiririko ya ukurasa wa 12 inaonyesha umuhimu wa UNDRIP katika kulinda haki za wenyeji na kuchangia katika maendeleo endelevu.

## NCHI 147 ZINZOUNGA MKONO UNDRIP

Afghanistan, Albania, Algeria, Andorra, Angola, Antigua na Barbuda, Argentina, Armenia, Australia, Austria, Bahamas, Bahrain, Barbados, Belarus, Belgium, Belize, Benin, Bolivia, Bosnia na Herzegovina, Botswana, Brazil, Brunei Darussalam, Bulgaria, Burkina Faso, Cambodia, Cameroon, Cape Verde, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chile, China, Colombia, Comoros, Congo, Costa Rica, Croatia, Cuba, Cyprus, Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Denmark, Djibouti, Dominica, Jamhuri ya Dominica, Ecuador, Misri, El Salvador, Estonia, Finland, Ufaransa, Gabon, Ujerumani, Ghana, Greece, Guatemala, Guinea, Guyana, Haiti, Honduras, Hungary, Iceland, India, Indonesia, Iran, Iraq, Ireland, Italia, Jamaica, Japani, Jordan, Kazakhstan, Kuwait, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao, Latvia, Lebanon, Lesotho, Liberia, Libyan Arab Jamahiriya, Liechtenstein, Lithuania, Luxembourg, Madagascar, Malawi, Malaysia, Maldives, Mali, Malta, Mauritius, Mexico, Nchi za Shirikisho za Micronesia, Moldova, Monaco, Mongolia, Msumbiji, Myanmar, Namibia, Nepal, Uholanzi, New Zealand, Nicaragua, Niger, Norway, Oman, Pakistan, Panama, Paraguay, Peru, the Philippines, Poland, Ureno, Qatar, Jamhuri ya Korea, Saint Lucia, Saint Vincent na the Grenadines, Samoa,

San Marino, Saudi Arabia, Senegali, Serbia, Sierra Leone, Singapore, Slovakia, Slovenia, Afrika Kusini, Spain, Sri Lanka, Sudan, Suriname, Swaziland, Sweden, Switzerland, Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Tanzania, Thailand, iliyokuwa Jamhuri ya Yugoslav ya Macedonia, Timor-Leste, Trinidad na Tobago, Tunisia, Turkey, United Arab Emirates, Uingereza, Uruguay, Venezuela, Vietnam, Yemen, Zambia na Zimbabwe.

Chanzo: www.un.org/esa/socdev/unpfii/en/declaration.html

# KIAMBATISHO CHA 2:

## MUUNDO WA KUFANYA UTAFITI WA SHERIA ZA NCHI KUHUSU FPIC

Maswali haya yameandaliwa kusaidia kuelewa iwapo haki yako ya Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha imelindwa katika sheria ya Taifa nchini kwako:

1. **Je,nchi yako imeonyesha kuunga mkono Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji (UNDRIP)??**

   Angalia orodha katika ukurasa wa 32 kuona iwapo nchi yako imeorodheshwa kama inaunga mkono UNDRIP. Kama haijaorodheshwa katika orodha hiyo kisha tazama katika Tovuti ya Umoja wa Mataifa: www.un.org/esa/socdev/unpfii/

2. **Je, kuna sheria yoyote katika sheria za taifa za nchi yako ambayo inaunga mkono FPIC?**

   KAMA NDIYO:

   Je, vifungu hivyo vinasemaje?

   Angalia kwa makini katika sheria kuona kinachotakiwa chini ya sheria hiyo.

   Inafanya kazi kwa nani?

   Angalia kuona iwapo sheria inaweza kutumika katika jamii zote zilizoathirika kutokana na mradi, au iwapo ni maalumu kwa Wenyeji.

   Je, ni hatua gani ambazo sheria inazitaka?

   Linganisha sheria za nchi yako katika Ibara ya 32 ya UNDRIP kuona iwapo kila kipengele cha FPIC kimezungumziwa. Tazama kwa karibu katika hatua zipi sheria imeweka.

   KAMA HAPANA:

   Kuna sheria yoyote katika sheria za taifa za nchi yako ambayo inaunga mkono michakato kama hiyo katika FPIC?

   Tazama iwapo nchi yako ina sheria ambayo imeweka michakato kama hiyo katika ya FPIC. Hii inaweza kuonekana katika sheria inayohusiana na maendeleo ya miundombinu m.f. mipango ya sheria.

   Je, michakato gani inayotakiwa chini ya sheria?

   Angalia kwa makini katika michakato iliyowekwa. Ni vipengele gani vya FPIC vinatakiwa katika sheria hiyo? Mifano inaweza kuhusisha: hatua za ushauri katika jamii, mahitaji ya mpango, mahitaji ya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii.

3. **Je, kuna sheria ya kesi yoyote katika nchi yako inayounga mkono Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha (FPIC)?**

   KAMA NDIYO:

   Je, mahakama iliamua nini?

   Tazama kesi ambazo jamii zilizoathirika kutokana na mradi zinazodai haki zake katika Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha katika sekta yoyote: machimbo ya madini, bwawa, ukataji wa magogo. Tazama kwa makini jambo ambalo mahakama ziliamua kwa kusoma hukumu zake.

   Je, inaweza kutumika katika kesi yako?

   Tazama mazingira ya kesi ambazo zinafanana na za kwako. Soma kuhusu kile ambacho mahakama ilisema. Je, sababu hizo zinaweza kutumika katika kesi yako.

   KAMA HAPANA:

   Je, kuna mfano wa kesi unaofanana na miradi ya nchini kwako?

   Kama hakujatokea kesi za mahakamani, fanya utafiti iwapo jamii zimekuwa zikiathirika na miradi mikubwa ya maendeleo. Walichukua hatua gani? Kunaweza kuwa na mifano ambayo inakusaidia kulinda haki zako. Je, kuna makundi ya jamii yanayochukua hatua dhidi ya miradi iliyopendekezwa katika nchi yako? Angalia iwapo asasi katika maeneo yako zina taarifa zaidi kuhusu wapi kwa kutafuta msaada kwa ajili ya michakato ya FPI.

# KIAMBATISHO CHA 3:

## MUUNDO WA MRADI

Miradi yote haifanani. Hata hivyo, miradi mikubwa inaweza kuwa na awamu zifuatazo. Mchoro ufuatao ni mwonekano wa jumla wa mzunguko halisi wa mradi. Unakusudia kusaidia kuelewa michakato iliyohusishwa unapojihusisha na waanzishaji wa mradi.

Mazoezi: Orodhesha nini hasa kinachotokea katika kila hatua ya mradi katika uanzishaji wa miundombinu mikubwa.

Shughuli za utendaji mzuri wa kuzishirikisha jamii: Hivi ndivyo waanzishaji wa mradi wanavyopaswa kufanya kuhakikisha jamii zinashirikishwa katika kila hatua ya mradi.

| AWAMU ZA MRADI | FPIC ilionyesha mambo muhimu katika kufanya uamuzi wakati wote wa mradi |
|---|---|
| WAZO LA MRADI | • Kubainisha fursa za mradi.<br>• Kibali kilichopatikana kutoka serikali za mitaa.<br>• Uchimbaji wa madini/utafiti wa mabwawa n.k |
| | • Kuzishirikisha jamii, kuwa wazi na kushauriana katika hatua za awali.<br>• Uchambuzi wa madhara yanayoweza kusababishwa na mradi ikiwa ni pamoja na masuala ya wadau.<br>• Kwa miradi migumu, kufanya mkutano wa mipango na wadau. |
| UPEMBUZI YAKINIFU NA MPANGO WA MRADI | • Waanzishaji wa mradi kupanga mradi.<br>• Tathmini za athari ya Kimazingira na Kijamii (ESIA) kufanyika. |
| | • Tathmini ya haki za binadamu inapaswa kufanyika.<br>• ESIA ina mpango wa kupunguza tatizo.<br>• Jadiliana na jamii kuhusu Makubaliano ya Faida yenye Madhara.<br>• Kuandaa pamoja na jamii hatua za kutatua malalamiko. |
| UJENZI | • Mwanzishaji wa mradi kuanza ujenzi wa mradi.<br>• Hii inaweza kuhusisha ununuzi wa ardhi, kusafisha ardhi, upangaji wa makazi mapya<br>• ya jamii n. |
| | • Jamii kufahamishwa kuhusu shughuli za ujenzi na kushauriwa kuhusu mabadiliko.<br>• Kuwepo kwa njia ya utatuzi wa malalamiko.<br>• Jamii zimefahamishwa vya kutosha kuhusu programu za uzuiaji wa athari za<br>• kimazingira na kijamii |
| UENDESHAJI | • Mpito kutoka ujenzi hadi uendeshaji.<br>• Kuanza kwa mifumo ya kusimamia uendeshaji. |
| | • Kuendelea kuwa wazi, kutoa ushauri na kuripoti kwa jamii zilizoathirika kutokana na mradi.<br>• Kuzuia ajali na uchafuzi kwa mujibu wa mipango ya usimamizi wa mazingira na jamii<br>• Utatuzi wa malalamiko yanayoendelea katika jamii. |
| KUONDOA KATIKA MATUMIZI | • Mradi kufikia mwisho.<br>• Waanzishaji wa mradi kuanza kuondoa au kufunga mradi. |
| | • Mipango ya kuondoa katika matumizi inahitaji kupitiwa na kuboreshwa, kwani<br>• wadau wanaweza kubadilika kutokana na mradi.<br>• Mpango na utekelezaji wa kushauriana na jamii (sawa na upembuzi yakinifu).<br>• Inapaswa kuwa sehemu ya ESIA. |



## NAFASI KWA AJILI YA MIHURI YA AISE

OXFAM